

NAMBA 3: MARKO 4:35-41: YESU ATULIZA DHORUBA: HABARI YA MAKARIPIO MATATU!

Hebu turejee katika injili ya Marko, na katika dakika chache, tutasoma **Marko sura ya nne**, mstari wa thelathini na tano, hadi mstari wa arobaini na moja. Ni kifungu maarufu sana, ambapo Yesu anatuliza dhoruba kwenye Ziwa Galilaya. Lakini kabla ya kusoma hiyo, nataka tuangalie kwa ufupi kile kilichotokea katika **sura ya tatu** - matukio yenye kuongoza hadi kifungu hiki. Unaposoma **sura ya tatu na nne** ya injili ya Marko, unaweza kuona kwamba, ulikuwa ni wakati wa shughuli nyingi sana kwa Yesu. Alikuwa juu mlimani akiomba kwa usiku mzima. Asubuhi iliyofuata aliwateua wanafunzi wake **kumi na mbili**, na akawaita Mitume. Na unaweza kuona orodha ya wanafunzi, katika mistari ya kumi na tatu hadi kumi na tisa, ya sura ya tatu. Wanafunzi kumi na moja walikuwa kutoka kaskazini mwa Israeli, kuzunguka eneo la Galilaya, na mmoja kutoka kusini - na huyo alikuwa ni **Yuda Iskariote**.

Kwa nini aliichagua kumi na mbili? Idadi hii ilikuwa takatifu kwa Wayahudi. Ilikuwa ni namba ambayo ilikuwa na maana kubwa katika historia yao. Katika Agano la Kale kulikuwa na mtu aliyetitwa **Yakobo** ambaye alikuwa na wana kumi na mbili. Wakawa familia kumi na mbili, na kisha wakawa makabila kumi na mbili – na tunajua kwamba makabila hayo, yakawa taifa la Israeli. Hivyo, ilikuwa namba maalum. Pia ilikuwa idadi ndogo ya watu katika kuwafundisha na kuwafunza. Ingekuwa vigumu kwa Yesu kufundisha mamia ya wanafunzi, na hivyo alichagua wanaume kumi na mbili tu, ili aweze kutumia muda pamoja nao, na kuwafundisha. Ambao wangeweza baadaye kuwa viongozi katika Kanisa la kwanza. Tunahitaji kukumbuka kwamba, kanisa lilianza na watu hawa, ingawa tunajua kwamba Yuda Iskariote baadaye alimsaliti Yesu, na kisha alienda kujua.

Wanafunzi hawa walikuwa ni kundi mchanganyiko la watu. Mmoja alikuwa mtoza ushuru. Mmoja alikuwa mkana-nayo - mtu aliyewapinga Warumi. Wengine wengi walikuwa ni wavuvi. Lakini tunachohitaji kuona ni kwamba walikuwa ni watu wa kawaida tu – hawakuwa watu maalum au muhimu. Yesu hakuwachagua kwa sababu walikuwa na elimu nzuri, au kwa sababu walikuwa matajiri. Aliwachagua watu wa kawaida, kama mimi na wewe, ili kuifanya kazi yake. Haya, neno 'Mtume' linamaanisha nini? Linamaanisha '*mtu aliyetumwa kwenda*'. Neno hili linaunganishwa na neno la Kiingereza 'mmisionari' au 'mjumbe'; mtu ambaye huenda sehemu za nje ili kuwaambia wengine injili. Kwa hiyo, Yesu aliwachagua wanafunzi wake kumi na mbili. Kisha akaenda Kapernaumu, ambako alikuwa na mahojiano na walimu wa sheria. Walikuwa wamemwona akitoa pepo kutoka kwa watu, lakini walimshutumu kuwa alikuwa akitoa pepo kwa kutumia nguvu za Shetani. Kama ukitazama **sura ya tatu, mstari wa ishirini na mbili**, utaona kile walichokuwa wakisema: "*Yeye amepagawishwa na Beelzebuli! Na kwa mkuu wa pepo, huwatoa pepo*". Kwa maneno mengine, nguvu alizokuwa akitumia Yesu zilikuwa hazitoki kwa Mungu, bali zilitoka kwa Shetani! Haya yalikuwa ni mashtaka makubwa. Kwa kweli, Yesu anaiita hiyo kuwa ni dhambi isiyosameheka. Naye anawaambia, "*inawezekaje Shetani kumfukuza Shetani? Na kama angefanya hivyo, basi ufalme wake utakuwa umegawanyika*".

Nina uhakika, hata katika mikusanyiko yetu, kuna watu wengi ambao wameuliza swali hili; Je, ni dhambi gani isiyosamehewa? Baadhi ya watu husema kwamba ni dhambi ya kujua, wakati ambapo mtu huamua kujua mwenyewe. La! Sivyo. Watu wengine wanasema, dhambi isiyosamehewa ni kitu kinachohusiana na kufanya ngono na uzinzi. La hasha, sivyo. Hizo ni dhambi mbaya, lakini sio dhambi zisizosameheka. Kama ukiangalia **sura ya tatu, mstari na ishirini na tisa na thelathini**, utaona jinsi ilivyo. "*Mtu yeyote anayekufuru dhidi ya Roho*

Mtakatifu hatasamehewa kamwe; ana hatia ya dhambi ya milele. Yesu alikuwa akisema hivyo kwa sababu walikuwa wakisema, ana roho mbaya". Kwa hiyo, hiyo ina maana gani? Dhambi isiyosameheka hutendwa, wakati mtu anaposema kwamba nguvu ya Roho Mtakatifu inatoka kwa Shetani - na mtu huyo huendelea kuamini hivyo.

Na haya ndiyo yaliwafanya walimu wa sheria kuwa na hatia. Kama mtu akiendelea kuamini kwamba mema ni maovu, hiyo ni dhambi ambayo haiwezi kusamehewa. Kama mtu akiyaona yale ambayo Mungu anafanya, naye akaendelea kusema '*Shetani ndiye anafanya hayo*' - hayo hayatasamehewa. Unaweza pia kusema, kama mtu akiendelea kutoziamini nguvu za Yesu, na akaendelea kuzikataa nguvu zake, dhambi hiyo haitasamehewa. Mtu huyo hatakubaliwa mbinguni. Kama mtu akiendelea kusema kwamba kazi ya Mungu ni kazi ya Shetani, hiyo ni dhambi ambayo haiwezi kusamehewa. Hiyo ni dhambi isiyosameheka ambayo Yesu anaizungumzia hapa.

Mara baada ya tukio hili, utaona kwamba mama na ndugu wa Yesu, walifika huko Kapernaumu, kutoka Nazareti, ili kumchukua Yesu na kumpeleka nyumbani. **Marko sura ya tatu, mstari wa ishirini na moja**, inasema kwamba walidhani kwamba Yesu "*alikuwa amerukwa na akili*". Walikuja kumchukua ili wampeleke nyumbani, kwa sababu walikuwa na wasiwasi naye. Hawakuelewa Misheni ya Yesu, na hivyo wao walipoona umati uliomfuata, na Mafarisayo wakimkataa, walifikiri kuwa walihitajika kumlinda. Sasa basi, baadaye katika Agano Jipya, tunajua kwamba mama yake, na mmoja wa ndugu zake (Yakobo) walikuja kuwa wafuasi wa Yesu, na wakiunga mkono huduma yake. Na kisha, katika **sura ya nne**, kama tulivyoona hapo awali, Yesu akaenda zake katika Ziwa Galilaya, na anaanza kufundisha kando ya ziwa, kutumia mifano: mfano wa mpanzi (ambao tulijifunza hapo awali); mfano wa taa juu ya kiango, mfano wa mbegu ya iliyopandwa na kukua, na mfano mbegu ya haradali. Na tunaambiwa katika **sura ya nne, mstari wa kwanza** kwamba, Yesu alikuwa akifundisha mifano hii akiwa katika mashua, kwa sababu ya umati uliokuwa ukimfuata, maana ulikuwa ni mkubwa sana.

Na hivyo, baada ya siku mbili za huduma yenye shughuli nyingi; akiomba na kufundisha; na kwa vile jioni nayo ilivyokuwa ikikaribia, tunamwona kwamba Yesu akiwa amechoka. Yesu alitaka kupumzika. Alitaka kutoka ili ajitenge na umati. **Mstari wa thelathini na tano**: "*wakati jioni alipowadia, aliwaambia wanafunzi 'twendeni tuvuke upande wa pili wa ziwa'*". Inasema: "*waliuacha umati, walimchukua Yesu, kama vile alivyokuwa, katika mashua*". Na huenda kwa kadiri mashua ilivyoanza kusafiri kutoka pwani, Yesu alijihisi unafuu pale anapouacha umati. Mwishowe, anapata muda kwa ajili ya amani na utulivu! Lakini, kumbuka kile kilichopo mwishoni mwa **mstari wa thelathini na sita**: "*Kulikuwa pia na mashua zingine pamoja naye!*"

Hakuweza kutoroka kutoka katika umati. Hata wakati alipokwenda kwenye ziwa, kulikuwa na watu ambao walitaka kumfuata katika mashua zao. Sasa, kifungu chetu haisemi kwamba Yesu alikuwa amechoka, lakini unayo haja ya kuangalia **mstari wa thelathini na nane** ili kuona kwamba Yesu alikuwa amechoka sana. Kulikuwa na uhitaji makubwa wa kumtaka yeye na huduma yake. "*Yesu alikuwa katika shetri ya mashua, amelala juu ya mto*".

Fikiria juu ya mstari huo. Inaonekana kuwa ya amani sana, sivyo? Ukiwa katika mashua. Ni wakati wa jioni njema. Maji yako katika utulivu, na mashua inasafiri kwa upole juu ya maji, nawe unaanza kusinzia. Inaonekana kuwa ni kitu kizuri! Na labda, ilikuwa ni wakati wa kuzama kwa jua katika ziwa, ndivyo jinsi ilivyokuwa wakati wao, walipoiacha pwani ya Kapernaumu. Lakini tunajua kwamba hali haikuendelea kuwa hivyo kwa muda mrefu. Ziwa

Galilaya liko juu kama **futi mia saba** kutoka kwenye usawa wa bahari, na lilikuwa limezungukwa na milima. Wakati mwingine, kwenye milima hii, upepo una nguvu sana. Na matokeo yake, hali ya hewa inaweza kubadilika haraka sana kwenye Ziwa Galilaya.

1. Nakumbuka nikiwa Galilaya miaka michache iliyopita. Tulikuwa tukiogelea katika ziwa wakati wa mchana mzuri, lakini tulipokuwa tayari kuondoka, mara upepo ukawa wa nguvu. Mawingu yalijaa, na kukawa na mvua nyingi. Haya yote yalitokea kwa ghafla sana. Kulikuwa ni amani na utulivu katika ziwa wakati dakika moja - lakini dakika chache baadaye, kulikuwa na upepo na mvua! Angalia katika **mstari wa thelathini na saba**: "*Ikatokea dhoruba kuu na upepo, na mawimbi yakaipiga mashua, nayo ilikuwa karibu na kuangamizwa*". Katika **Injili ya Mathayo**, inasema: "*bila ya onyo, dhoruba kali ilikuja juu ya ziwa*". Mathayo anatumia neno la Kiyunani kuelezea dhoruba – na neno analolitumia ni '*tetemeko la ardhi*'. Kwa maneno mengine, hii ilikuwa dhoruba kali. Na katika mashua, aliyokuwamo Yesu, na wanafunzi wake kumi na mbili. Na kumbuka, baadhi ya wanafunzi hawa walikuwa ni wavuvi wazoefu na wataalamu.

Wanalijua ziwa, na wanajua jinsi ya kuongoza mashua. Lakini dhoruba hii lazima ilikuwa ni mbaya sana, kwa sababu wao wameogopa, na wameingiwa na hofu – pale upepo unavyoipiga mashua, na mawimbi yanaingia kwa juu katika upande wa mashua. Wakati huo huo, kwa namna fulani, Yesu alikuwa amelala kwa haraka nyuma ya mashua! Sasa, najua baadhi ya watu wanaweza kusinzia mahali popote, na kwa wakati wowote, bila kujali kinachoendelea karibu nao - lakini hii ni ajabu, si hivyo?! Je, ni kwa namna gani Yesu alikuwa amelala? Nafikiri ni kwa sababu Yesu alikuwa amechoka sana kutokana na mahitaji ya huduma yake. Alikuwa amechoka sana. Na hii inaweza kweli kuwa ni jambo la kutia moyo kwetu kama Wakristo. Injili ya Marko imejawa na miujiza. Wagonjwa wanaponywa. Wenye pepo wanafunguliwa. Samaki na mkate inaongezwa, na dhoruba inatulizwa. Mambo haya yote yanaonyesha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, na kwamba anaweza kufanya yasiyo-wezekana. Lakini nafikiri kwamba Marko anatumia sisi kuona kwamba, Yesu ni mwanadamu pia.

Yesu ni Mwana wa Mungu, lakini wakati ule alipokuja duniani, alifanyika mtu. Alikuwa binadamu, na alikuwa na uzoefu huo wa hisia za binadamu kama sisi. Kwa hiyo, hapa katika kifungu chetu, tunaona ubinadamu wa Kristo. Akiwa amechoka sana. Hawezi kukaa macho bila kufumba. Je, unakumbuka kisa cha mwanamke katika Samaria? Tunasoma katika injili ya **Yohana** kwamba Yesu alikuwa amechoka baada ya safari ndefu. Alikuwa ametembea kwa kilometa nyingi, na hivyo alikaa chini karibu na Kisima cha Yakobo. Halafu akamwomba mwanamke maji ya kunywa. Hiyo inatuonyesha kuwa yeye aliona kiu. Kumbuka, katika kaburi la **Lazaro**, tunasoma kwamba Yesu alilia kwa sababu ya kifo cha rafiki yake.

Yesu alikuwa mtu ambaye alilia! Injili inatuonyesha kwamba Yesu ni binadamu kamili.

Waebrania sura ya nne, mstari wa kumi na tano, inasema kuwa tuna kuhani mkuu, ambaye ana uwezo wa kuchukuliana na udhaifu wetu, kwa sababu alijaribiwa katika kila njia, kama vile tunavyojaribiwa - na bado hakufanya dhambi. Huu ni ubinadamu wa Kristo. "*Yesu alikuwa nyuma ya mashua, amelala na kichwa chake amekilaza juu ya mto*". Hivyo ndivyo alivyokuwa amechoka katika hatua hii.

Na kisha tunaona karipio la kwanza kati ya matatu. Angalia mwisho wa **mstari thelathini na nane**: Wanafunzi wanaogopa. Wanahofia maisha yao. Hivyo nadhani mmoja wa wanafunzi alimwamsha Yesu kwa kumgusa mabega: "*Mwalimu, Je, haujali kuwa sisi tunazama?*" "*Je, wewe haujali?*" Ni swali la namna gani la kumwuuliza Mwana wa Mungu! Yesu ambaye hivi karibuni angekufa msalabani, na kuyatoa maisha yake kwa ajili ya watu. Bila shaka yeye anajali! Walikuwa wamemwona katika akitenda mara nyingi, akijali watu katika kiwango cha

kimwili na kiroho. Hawakuhitaji kumkemea Yesu. Wanapaswa kujua wangekuwa salama pamoja naye. Lakini kwa sababu ya hofu zao na masumbufu yao; walikuwa hawafikirii vizuri. Hofu ilikuwa imetawala na kuwadhibiti. Na kipindi linatokea jambo kama hili, unanza kufikiria na kusema mambo ambayo si ya kweli. "*Yesu, Je, wewe haujali*"?

Je, umewahi kuwa katika nafasi kama hiyo? Labda unapitia kwenye dhoruba katika maisha yako sasa hivi. Sizungumzii juu ya dhoruba ya kimwili, ambapo kuna mvua nyingi na upepo, na radi. Ninazungumzia kuhusu ugumu maishani mwako. Labda unaweza kufikiria juu ya dhoruba katika siku za nyuma ambayo uliipitia. Labda ulikuwa na afya mbaya. Labda kuna mtu katika familia yako alifariki. Labda ulikuwa na shida katika maisha yako, au katika Kanisa. Nina uhakika kuwa sisi sote tumekuwa katika dhoruba katika maisha yetu. Na wakati mwingine, tunapopita katika nyakati hizo ngumu, tunaweza kujaribiwa kuuliza swali sawa na lile ambalo wanafunzi waliuliza. "*Bwana, Je, haunijali mimi*"? "*Je unaweza kuona yale ambayo ninayapitia*"? Tunajihisi kama tuko sisi wenyewe tu katika dhoruba, na kwamba Mungu hatujali. Ikiwa ndio wewe, unahitaji kujua kwamba Mungu anakujali. Yeye anakijua zaidi hicho unachokipitia. Anakijua unacho-kifikiria. Anajua kila wimbi ambalo linakugonga.

Barua ya kwanza ya Petro, sura ya tano, mstari wa saba inasema hivi: "*Mtwishe fadhaa zako zote, kwa sababu Yeye anakujali – anaji-shughulisha ajili yako*". Anajua; anaona, na anajali. Hata kama hatuwezi kuhisi, ni katika kipindi cha dhoruba ambacho Mungu hutufundisha kuhusu yeye mwenyewe. Wanafunzi katika **Marko sura ya nne** - wanaogopa, na hawakujua kwamba Yesu hatumia dhoruba hii, kuwafundisha kuhusu Mungu na uwezo wake katika maisha yao. Dhoruba ilihitajika kwa ajili ya ukuaji wao wa kiroho. Kama hakutakuwa na shida katika maisha yetu, hatungeweza kukua ili kuwa Wakristo waliokomaa. Dhoruba ni sehemu ya mchakato wa ukuaji wa kiroho. Wakristo wengi wanaweza kusema kwamba, wamekua katika Kristo kwa sababu ya ugumu na matatizo. Wamejifunza kumwamini Mungu katika dhoruba za maisha, hata kama wakati huo, hawakupenda. Tuna uwezo wa kukua katika imani, kwa sababu ya dhoruba. Na kwa sababu tu Yesu anaonekana kuwa amelala, wakati sisi tukiteseka, haina maana kuwa yeye hajali.

Hebu tuendeleo kwenye karipio la pili. Angalia katika **mstari wa thelathini na tisa**: Yesu ameamshwa kutoka usingizini. Anainuka, na kuukemea upepo, naye anayaamuru mawimbi kuwa kimya na tulivu. Na nini kinatokea? "*Upepo alikoma, na kulikuwa na shwari kuu*". Upepo umekoma mara moja! Mara tu Yesu alipoikemea dhoruba, kwa amri yake, kila kitu kilitulia na kuwa kimya. Mawimbi yalishushwa chini, na upepo haukuwepo tena. Na lazima kuwe na ukimya wa ajabu! Je, unaweza kufikiria je namna ilivyokuwa? Kulikuwa na upepo mkali sana, na maji yanaingia mashua - na kisha ghafla, kuna utulivu kamili na amani. Wanafunzi walikaa huko, wakitazama kila mtu na mwingine kwa kutokuamini. **Mstari wa arobaini na moja** unatuambia kuwa walikuwa na hofu. Waliuliza, "*Ni nani huyu? Hata upepo na mawimbi humtii*". Na katika wakati huo, ingawa walikuwa wameona miujiza mingine, ghafla walitambua kwamba, Yesu alikuwa Mungu mwenyewe.

Hatujui, lakini huenda walikumbuka vifungu katika Agano la Kale, ambavyo vinamtaja Mungu kuwa katika udhibiti wa bahari. Kuna Zaburi chache zinazomtaja Mungu akituliza bahari, na kukemea maji. Zinatuonyesha Mungu Muumba, ambaye ndiye mwenye dhamana ya uumbaji wake. **Zaburi themanini na tisa, mstari wa tisa** inasema haya: "*Wewe utawalaye juu ya kiburi cha bahari. Na mawimbi yake yainukapo, wewe huyatuliza*". **Zaburi mia moja na nne, mstari wa saba**: "*katika kukemea kwako maji yakimbia*". Labda waliyakumbuka maneno ya **Zaburi mia moja na saba**. Hebu na tuirejee Zaburi hiyo, na tusome mistari michache. Na

tunaposoma maneno haya, fikiria jinsi yanavyowafaa wanafunzi hawa (mistari ya ishirini na nne hadi thelathini). Aisee! Mistari hii inaonekana kuelezea hali ya wanafunzi kumi na mbili, sivyo? Je, unadhani kwamba wanafunzi waliikumbuka Zaburi hii walipokuwa wamekaa ndani ya mashua?

Hatujui, lakini walipokuwa wameketi kwenye mashua, na kushuhudia dhoruba ilivyotulizwa, Bibilia inafanywa kuwa hai na halisi mbele ya macho yao! Je, mtu huyu ni nani? Huyu ni Mungu mwenyewe. Macho yao yakafumbuliwa, na walimwona Yesu kwa kweli. Huko ndani ya mashua walikuwa pamoja nao, na Mwana wa Mungu; mtu aliyeumba ulimwengu wote. Hakuna mwingine anayeweza kudhibiti maji na upepo kwa namna hii. Ni lazima awe Mungu. Kumbuka kile ambacho **Paulo** alikiandika katika **Kitabu cha Wakolosai**: *"Kwake yeye vitu vyote viliumbwa; vitu vya mbinguni na vya duniani, vinavyoonekana na visivyoonekana; vitu vyote waliumbwa naye, na katika yeye vitu vyote vinashikiliwa kwa pamoja"*. Muumba wa dunia anaweza kudhibiti uumbaji wake. Huu ni wakati wa ajabu kwa wanafunzi. Huyu hapa ni Mungu pamoja nao katika mashua yao ndogo! Jamani!

Na kisha, tunafikia mwisho wa kifungu, tuangalie karipio la tatu. **Mstari wa arobaini**: Karipio la kwanza: Wanafunzi wamemkemea Yesu. Karipio la pili: Yesu ameikemea dhoruba. Na sasa, karipio la tatu, Yesu anawakemea wanafunzi wake: *"Kwa nini mna hofu? Kwa nini mnaogopa? Je, bado hamna imani?"* Je, hii inamaanisha nini kwa wanafunzi? Yesu akawaambia, kama mimi ni Mwana wa Mungu; kama mimi ni Muumba wa ulimwengu, basi ninaweza, na nitatimiza mahitaji yako yote. Iweni na imani nami. Weka matumaini yako kwangu. Usiiruhusu hofu itawale maisha yako. Mimi niko katika mashua pamoja na wewe, nami nitakujali wewe. Msiogope! Na neno hilo linatumika sana katika Biblia. Labda kwa sababu sisi ni binadamu tu, Mungu anajua kwamba mara nyingi hofu na wasiwasi hutawala maisha yetu. Msiogope, Mimi ni pamoja nanyi.

Fikiria juu ya hili. Kanisa ni kama mashua kwenye dhoruba ndani ya maji. Kanisa, kama mashua, hupitia nyakati ngumu. Wakati mwingine kuna mateso katika Kanisa. Wakati mwingine kuna mgawanyiko katika Kanisa. Wakati mwingine huonekana kama Kanisa litaharibiwa. Lakini, nyuma ya mashua kuna Yesu, ambaye ni mkuu wa Kanisa. Yeye yu pamoja nasi wakati wote. Kwa kweli, si kwamba yu pamoja nasi tu, lakini kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, yeye yu ndani yetu! Na hiyo inamaanisha, hata kama kuna hatari, wakati dhoruba na matatizo yanapokuja, kama tutamruhusu, tunaweza kuishi maisha yetu kwa amani, ambayo ni zaidi ya uelewa wa kibinadamu.

Acha nikwambie habari kumhusu kaka yangu **Filipo**, ambaye alikuwa akifanya kazi katika jeshi. Kazi yake ilikuwa katika helikopita ya jeshi. Alilazimika kwenda Afghanistan kusaidia majeshi katika vita. Haya ndiyo anayoyasema: *tulikuwa juu katika anga kusubiri mapigano yatulie huko chini, ili tuweze kusafiri na kuwaokoa askari waliojeruhiwa. Nakumbuka nilijawa na hisia za uoga sana pale tulipokuwa tunapaa huku tukisubiri - na kisha, pale helikopita iliposhuka chini haraka sana kuelekea ardhini, hofu yangu iliongezeka. Katika hatua hii mwili wangu wote ulikuwa na hofu - lakini ninaweza kukumbuka kuwa ilikuwa katika hatua hii jambo la kushangaza lilitokea. Nilikuwa sijamwomba Mungu ili aondoe, lakini ilitokea tu. Nilihisi amani ya ajabu ikiingia mwilini mwangu, kutoka vidole vyangu - hadi utosini juu ya kichwa changu. Hata kama tulikuwa tunapaa katika uwanja wa vita, ili kuangalia wanajeshi waliojeruhiwa, na ingawa kulikuwa na risasi zikipigwa karibu, hofu yote ilikuwa imekwisha, na nilikuwa na amani kamili"*.

Je, kisa hicho kinatuambia nini? Hata kama unapitia katika shida, jua kuwa Mungu yupo kwa ajili yako. Mungu anasema mara nyingi katika Biblia. Usiogope, kwa kuwa Mimi ni pamoja nawe. Nitaleta amani katika nyakati ngumu, kama utaniruhusu. Je, Yesu aliwaambia nini wanafunzi? *"Kwa nini mna hofu? Kwa nini mnaogopa? Je, bado hamna imani?"* Je, tumejifunza somo hilo? Wakati upepo unapovuma katika maisha yetu; wakati matatizo yanapotupata, Je, tumejifunza kumwamini? Je, tumejifunza kusema kuwa *'Nitatumaini katika Bwana huyu'*? Au tunaruhusu uoga ututawale? Labda hofu na wasiwasi ni suala, ambalo tunakumbana nalo mara nyingi. Labda una wasiwasi juu ya afya yako, au una wasiwasi kuhusu pesa, au kuhusu huduma yako. Huenda upepo unapuliza sasa hivi katika maisha yako, na huna matumaini sana.

Kumbuka kwamba Kristo yuko kwenye mashua pamoja nanyi. Unahitaji kujua kwamba anakujali. Anakuona. Yeye anaweza kukuokoa kutoka katika maji kwa neno rahisi kama atataka. Elewa kwamba Mungu anakutaka ukue katika dhoruba, na kwamba anataka wewe umwamini kabisa. Wakati imani yetu ikiwa hai na tunamtumaini Yeye, hofu itapotea, na amani itakuja. **Zaburi ishirini na saba, mstari wa sita** inasema hivi: *"Bwana yu pamoja nami; hivyo mimi sitakuwa na hofu"*. Baba Mungu, tusaidie kuyaweka maneno haya katika matendo. Tusaidie kukuamini wewe. Tusaidie sisi tusiwe na hofu, hata wakati tunapopita katika nyakati ngumu.
